ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI

ZANZIBAR

		MHE. ZUBEIR ALI MAULID	**-**	**SPIKA**
1.	**Mhe.**	**Abdalla Ali Kombo**	**-**	**Jimbo la Mwanakwerekwe**
2.	**Mhe.**	**Abdalla Maulid Diwani**	**-**	**Jimbo la Jang'ombe**
3.	**Mhe.**	**Ali Khamis Bakar**	**-**	**Jimbo la Tumbe**
4.	**Mhe.**	**Ali Salum Haji**	**-**	**Jimbo la Kwahani**
5.	**Mhe.**	**Ali Suleiman Ali (Shihata)**	**-**	**Jimbo la Kijitoupele**
6.	**Mhe.**	**Ame Haji Ali**	**-**	**Jimbo la Nungwi**
7.	**Mhe.**	**Amina Iddi Mabrouk**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
8.	**Mhe.**	**Asha Abdalla Mussa**	**-**	**Jimbo la Kiwengwa**
9.	**Mhe.**	**Bahati Khamis Kombo**	**-**	**Jimbo la Chambani**
10.	**Mhe.**	**Bihindi Hamad Khamis**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
11.	**Mhe.**	**Chum Kombo Khamis**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
12.	**Mhe.**	**Haji Omar Kheri**	**-**	**Jimbo la Tumbatu**
13	**Mhe.**	**Hamad Abdalla Rashid**	**-**	**Jimbo la Wawi**
14.	**Mhe.**	**Hamida Abdalla Issa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
15.	**Mhe.**	**Hamza Hassan Juma**	**-**	**Jimbo la Shaurimoyo**
16.	**Mhe.**	**Haroun Ali Suleiman**	**-**	**Jimbo la Makunduchi**
17.	**Mhe.**	**Harusi Said Suleiman**	**-**	**Jimbo la Wete**
18.	**Mhe.**	**Hassan Khamis Hafidh**	**-**	**Jimbo la Welezo**
19.	**Mhe.**	**Hidaya Ali Makame**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
20.	**Mhe.**	**Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)**	**-**	**Jimbo la Mtoni**

21.	**Mhe.**	**Issa Haji Ussi (Gavu)**	**-**	**Jimbo la Chwaka**
22.	**Mhe.**	**Jaku Hashim Ayoub**	**-**	**Jimbo la Paje**
23.	**Mhe.**	**Juma Makungu Juma**	**-**	**Jimbo la Kijini**
24.	**Mhe.**	**Khadija Omar Kibano**	**-**	**Jimbo la Mtambwe**
25.	**Mhe.**	**Dkt. Khalid Salum Mohamed**	**-**	**Jimbo la Donge**
26.	**Mhe.**	**Khamis Juma Mwalim**	**-**	**Jimbo la Pangawe**
27.	**Mhe.**	**Lulu Msham Abdalla**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
28.	**Mhe.**	**Machano Othman Said**	**-**	**Jimbo la Mfenesini**
29.	**Mhe.**	**Mahmoud Thabit Kombo**	**-**	**Jimbo la Kiembesamaki**
30.	**Mhe.**	**Dkt. Makame Ali Ussi Makoti**	**-**	**Jimbo la Mtopepo**
31.	**Mhe.**	**Makame Said Juma**	**-**	**Jimbo la Kojani**
32.	**Mhe.**	**Maryam Thani Juma**	**-**	**Jimbo la Gando**
33.	**Mhe.**	**Masoud Abrahman Masoud**	**-**	**Jimbo la Bububu**
34.	**Mhe.**	**Mgeni Hassan Juma**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
35.	**Mhe.**	**Mihayo Juma N'hunga**	**-**	**Jimbo la Mwera**
36.	**Mhe.**	**Miraji Khamis Mussa**	**-**	**Jimbo la Chumbuni**
37.	**Mhe.**	**Mmanga Mjengo Mjawiri**	**-**	**Jimbo la Mkoani**
38.	**Mhe.**	**Moh'd Mgaza Jecha**	**-**	**Jimbo la Mtambile**
39.	**Mhe.**	**Mohamed Ahmada Salum**	**-**	**Jimbo la Malindi**
40.	**Mhe.**	**Mohammed Said Mohammed**	**-**	**Jimbo la Mpendae**
41.	**Mhe.**	**Mohammedraza Hassanaali Mohamedali**	**-**	**Jimbo la Uzini**
42.	**Mhe.**	**Mtumwa Peya Yussuf**	**-**	**Jimbo la Bumbwini**
43.	**Mhe.**	**Mtumwa Suleiman Makame**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
44.	**Mhe.**	**Mussa Ali Mussa**	**-**	**Jimbo la Ole**

45.	**Mhe.**	**Mussa Foum Mussa**	**-**	**Jimbo la Kiwani**
46.	**Mhe.**	**Mwanaasha Khamis Juma**	**-**	**Jimbo la Chukwani**
47.	**Mhe.**	**Mwanaidi Kassim Mussa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
48.	**Mhe.**	**Mwantatu Mbaraka Khamis**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
49.	**Mhe.**	**Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini**	**-**	**Jimbo la Dimani**
50.	**Mhe.**	**Nadir Abdul-latif Yussuf**	**-**	**Jimbo la Chaani**
51.	**Mhe.**	**Nassor Salim Ali**	**-**	**Jimbo la Kikwajuni**
52.	**Mhe.**	**Omar Seif Abeid**	**-**	**Jimbo la Konde**
53.	**Mhe.**	**Panya Ali Abdalla**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
54.	**Mhe.**	**Rashid Ali Juma**	**-**	**Jimbo la Amani**
55.	**Mhe.**	**Rashid Makame Shamsi**	**-**	**Jimbo la Magomeni**
56.	**Mhe.**	**Riziki Pembe Juma**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
57.	**Mhe.**	**Saada Ramadhan Mwenda**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
58.	**Mhe.**	**Said Omar Said**	**-**	**Jimbo la Wingwi**
59.	**Mhe.**	**Salama Aboud Talib**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
60.	**Mhe.**	**Said Hassan Said**	**-**	**Mwanasheria Mkuu**
61.	**Mhe.**	**Salha Mohamed Mwinjuma**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
62.	**Mhe.**	**Salma Mussa Bilal**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
63.	**Mhe.**	**Balozi Seif Ali Iddi**	**-**	**Jimbo la Mahonda**
64.	**Mhe.**	**Shadya Mohamed Suleiman**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
65.	**Mhe.**	**Shaib Said Ali**	**-**	**Jimbo la Chonga**
66.	**Mhe.**	**Shamata Shaame Khamis**	**-**	**Jimbo la Micheweni**
67.	**Mhe.**	**Shehe Hamad Mattar**	**-**	**Jimbo la Mgogoni**
68.	**Mhe.**	**Simai Mohammed Said**	**-**	**Jimbo la Tunguu**

69.	**Mhe.**	**Suleiman Makame Ali**	**-**	**Jimbo la Ziwani**
70.	**Mhe.**	**Suleiman Sarahan Said**	**-**	**Jimbo la Chakechake**
71.	**Mhe.**	**Tatu Mohamed Ussi**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
72.	**Mhe.**	**Ussi Yahya Haji**	**-**	**Jimbo la Mkwajuni**
73.	**Mhe.**	**Viwe Khamis Abdalla**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
74.	**Mhe.**	**Wanu Hafidh Ameir**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
75.	**Mhe.**	**Yussuf Hassan Iddi**	**-**	**Jimbo la Fuoni**
76.	**Mhe.**	**Zaina Abdalla Salum**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
77.	**Mhe.**	**Zulfa Mmaka Omar**	**-**	**Nafasi za Wanawake**

	Dkt. Yahya Khamis Hamad	**-**	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

BARAZA LA WAWAKILISHI - ZANZIBAR

BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KWANZA

Kikao cha Kwanza - Tarehe 30 Machi, 2016

(Kikao kilianza Saa 3.00 Asubuhi)

WIMBO WA TAIFA WA ZANZIBAR

DUA

Katibu *(Dkt. Yahya Khamis Hamad) alisoma Dua*

TANGAZO LA KUITISHA MKUTANO WA BARAZA

Katibu: Waheshimiwa Wajumbe kwa mujibu wa Kanuni ya 20 inaelezea kwamba bila ya kuathiri masharti ya Katiba Mkutano wa kwanza wa Baraza jipya utaanzishwa tarehe ile ambayo Baraza jipya limeitishwa na Mhe. Rais.

Kanuni ya 21(2) inanitaka nisome hilo Tangazo la Mhe. Rais. Kwa heshima na taadhima sasa naomba nilisome tangazo hilo ambalo linasomeka kama ifutavyo.

Hati ya kuitisha Mkutano wa Baraza la Wawakilishi chini ya kanuni ya 91 ya Katiba 91 kifungu kidogo cha kwanza cha Katiba, tangazo lenyewe limetolewa kama ifuatavyo:

"Mimi Dk. Ali Moh'd Shein Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uwezo niliopewa chini ya kifungu cha 91(1) cha Katiba ya Zanzibar ya 1984, naamuru kwamba Mkutano wa Baraza la Wawakilishi ufanyike kwa ajili ya kuendelea na shughuli zake kuanzia tarehe 30 Machi, 2016 saa 3:00 asubuhi."

Tangazo hilo lilisainiwa na Mhe. Rais Dk. Ali Moh'd Shein tarehe 26 Machi, 2016.

UCHAGUZI WA MHE. SPIKA

Katibu: Waheshimiwa Wajumbe kwa mujibu wa Katiba kiti cha Spika, hakitakiwi kiwe wazi kwa muda wowote ule ambao Baraza litakutana, na kadri mnavyojua ndio kwanza tumetoka kwenye uchaguzi kiti cha Spika kiko wazi kwa hivyo jambo la kwanza ambalo tunatakiwa tulifanye kwa mujibu wa Katiba ni kumchagua Spika wa Baraza hili Tukufu.

Waheshimiwa Wajumbe kutoka Tume ya Uchaguzi ambako tulipeleka taarifa kwamba Wajumbe wa Vyama vyote vyenye usajili wa kudumu vinaweza kupeleka mgombea wa kiti hiki, hadi tunapokaa saa hizi tumepokea jina la mgombea mmoja tu wa Chama cha Mapinduzi ambaye ni Mhe. Zubeir Ali Maulid, ndiye ambaye jina lake limependekezwa kwetu kwa ajili ya uchaguzi huo.

Kwa heshima na taadhima naomba sasa nimuite Mhe. Zubeir Ali Maulid aje mbele yetu kuwasalimia. Kwa mujibu wa Kanuni atakuwa na dakika tano za kuzungumza nanyi, na baada ya mazungumzo yake, na kama akiamua kuzungumza basi Waheshimiwa Wajumbe mtapata nafasi ya kuuliza maswali matatu, ni maswali matatu. Kanuni haijasema kama yaulizwe na watu watatu kwa hivyo mkiruhusu mtu mmoja aulize matatu yatakuwa maswali matatu yamepita lakini kwa kawaida haturuhusu swali moja zaidi ya mtu mmoja, ni pale ambapo mwenyewe ataamua kuzungumza akisema anaamua tu mumuachie kwanza atazungumza baadae anaweza kufanya hivyo.

Sasa kwa heshima na taadhima nawaomba watendaji wenzangu wanitafutie Mhe. Zubeir Ali Maulid popote alipo wamlete sasa kwa ajili ya shughuli hii ya uchaguzi.

(Hapa watendaji walikwenda kumtafuta Mhe. Zubeir Ali Maulid mgombea wa Uspika:

(Watendaji wa Baraza waliingia na Mhe. Zubeir Ali Maulid ndani ya ukumbi wa Baraza la Wawakilishi)

Katibu: Mhe. Zubeir Ali Maulid kwa heshima na taadhima tunapenda kukujulisha kwamba wewe ni mgombea pekee wa kiti cha Spika wa Baraza la Wawakilishi.

Kwa mujibu wa kanuni zetu sasa hivi ni wakati wa kufanya uchaguzi kwa ajili ya kuchagua Spika, ili wajumbe wapate nafasi ya kuelezea hisia zao juu yako kwa kipitia uchaguzi, muda huu tulionao Mheshimiwa kwa mujibu wa kanuni una nafasi ya kuzungumza kwa muda wa dakika tano kuwaeleza wajumbe lile ambalo unapenda wakusikie katika hatua hii, na si zaidi ya dakika tano, na kama utaamua kuzungumza hiyo ni hiyari yako, ukiamua kuzungumza basi Wajumbe watapata nafasi ya kukuuliza maswali yasiyozidi matatu, baada ya hapo tutaingia kwenye hatua ya uchaguzi. Mheshimiwa karibu sana.

(Hapa Mhe. Zubeir Ali Maulid Mgombea Uspika alipanda juu na kujinadi kwa kuomba kura)

Mhe. Zubeir Ali Maulid: Waheshimiwa Wajumbe kwanza *Assalamu alaykum*. Niliyesimama mbele yenu naitwa Zubeir Ali Maulid, na kwa bahati nzuri Mwenyezi Mungu kajaalia kwamba nakuwa mgombea pekee wa kiti hichi cha Uspika, na kwa vile nipo peke yangu sina haja ya kuwa na mazungumzo marefu sana ya kukuchosheni.

Nimesimama mbele yenu kukuombeni kura zenu zote ili muweze kunithibitisha kuwa Spika wenu, na nakuahidini kuwa tutafanya kazi kwa pamoja kwa mashirikiano ya hali ya juu na nitakuwa msikivu, nitakuwa nashaurika, tutashauriana vizuri ili tuweze kuendesha chombo hichi ili wananchi waweze kupata kile ambacho wanakitegemea kutoka kwetu sote kwa pamoja.

Waheshimiwa Wajumbe kwa hayo machache nakwambieni kwamba naomba kura zenu. *(Makofi)*

Katibu: Waheshimiwa tuna nafasi tatu za maswali kama mkipenda.

Waheshimiwa Wajumbe: Hakuna!

Katibu: Mheshimiwa unaweza kwenda *(Makofi)*

(Mhe. Zubeir Ali Maulid alitoka nje ya ukumbi kwenda kusubiri zoezi la uchaguzi)

Katibu: Waheshimiwa Wajumbe sasa hatua inayofuata ni uchaguzi wa Spika, kanuni inasema kura zitakuwa za siri na naomba watendaji wenzangu wafunge mlango tuhesabu Wajumbe waliopo tujue idadi yao halafu tuanze kura. Waheshimiwa kwa ruhusa yenu tunaanza hilo zoezi.

Waheshimiwa tulitegemea tuwe na wajumbe 77 ndani ya ukumbi sasa hivi, lakini wapo 76 hata hivyo hiyo isingezuia vyovyote kwa sababu kanuni zinasema mshindi atapatikana kwa wajumbe waliopo na kupiga kura na hata hivyo ni mmoja tu hayupo nashukuru sana ni hatua kubwa mno kwa sababu hatujui hiyo dharura ya huyo mmoja ikoje.

Tutakavyofanya Waheshimiwa Wajumbe sasa hivi tutagawa karatasi za kupigia kura, karatasi hizo kwa sababu kuna mgombea mmoja kama mlivyoona litaonekana jina la Mhe. Zubeir Ali Maulid wa Chama cha Mapinduzi na chini yake kuna sehemu ya ndio na hapana, tutaomba kila mjumbe atapewa karatasi moja ya kura na tutaomba aoneshe alama ya ndio au hapana, isiwe ndio na hapana, atie moja katika mbili hizo baadae tuchukue hizo kura na

kuzihesabu, kama nilivyotangulia kusema ni kwamba baada ya zoezi hilo tutahesabu kura na mshindi atapatikana kwa kura nyingi za waliopiga kura.

Waheshimiwa kwa heshima na taadhima naomba watendaji wenzangu sasa waanze kugawa karatasi za kupigia kura, naomba muoneshe kwamba masanduku hayana kitu na yapo matupu kabisa na hizo ni nakiri ambazo tutayafunga baada ya kura kupigwa, karatasi halisi Waheshimiwa tumepiga mihuri nyuma, kama haina muhuri hiyo siyo, kanuni inasema hivyo. Naomba mukae vilevile mulivyo tutapitisha maboksi yetu ahsanteni.

Baada ya kukusanya hizo kura Waheshimiwa tutaahirisha Baraza kama mnavyojua sasa hivi tupo ndani ya Baraza tutaahirisha Baraza kwa muda wa nusu saa kwa kwenda kuhesabu kura na baadae tutarudi kwa kuwatangazia matokeo ya kura.

Waheshimiwa Wajumbe naomba sana kama kuna Mjumbe hajapata karatasi ya kupigia kura basi anijulishe.

Naomba mtendaji mmoja aende kwa Mhe. Zubeir Ali Maulid atwambie ni nani angependa asimamie kuona kura zake wakati zinahesabiwa, naomba haraka sana tupate hilo jibu ili tuanze hili zoezi, aseme ni mjumbe gani anapenda asimamie kwa niaba yake wakati kura zake zinahesabiwa.

Mhe. Zubeir Ali Maulid mgombea kiti cha Uspika, amemteua Mhe. Hamza Hassan Juma kusimamia kuhesabu kura, naomba watendaji wawili waje kubeba chini ya usimamizi wangu na Mhe. Hamza Hassan Juma naomba mje mchukue, na Mhe. Hamza naomba uandamane nao na mimi nakuja.

Waheshimiwa Wajumbe kwa mujibu wa Kanuni za Baraza zinaonesha kwamba baada ya kukusanywa kura Baraza linaweza kuahirishwa kwa muda wa nusu saa ili kura zikahesabiwa na baada ya nusu saa Baraza litarudia kwa kutangaza matokeo na kuapishwa Spika aliyechaguliwa.

(Saa 3:18 Baraza liliahirishwa kwa kuhesabu kura)

(Saa 3:50 Baraza lilirudia)

Katibu: Waheshimiwa Wajumbe naomba mukae. Waheshimiwa Wajumbe, kwa heshima na taadhima naomba nitoe taarifa kwamba zoezi la kuhesabu kura limemalizika na limekwenda vizuri.

Kama tulivyosema awali kura zilizopigwa zilikuwa ni 76, kati ya kura hizo ni kura 1 tu ambayo imeharibika, na namna ilivyoharibika ni kwamba mjumbe amerudisha bila ya kuweka alama mahali popote, hivyo ndivyo ambavyo kura imeharibika. Kura nyengine zilizobaki ni 75 na kura zote hizo zimewekwa kwenye alama ya ndiyo. Kwa maana hiyo ni kwamba hakuna kura ambayo imemkataa mgombea wa Uspika ambaye alikuwa anachaguliwa sasa hivi, na kwa hatua hiyo naomba nichukue nafasi hii rasmi kumtangaza Mhe. Zubeir Ali Maulid wa Chama cha Mapinduzi kuwa ameteuliwa kuwa ni Spika wa Baraza la Tisa. (*Makofi*)

Mhe. Zubeir Ali Maulid sasa ndiye Spika wa Baraza la Tisa la Wawakilishi la Zanzibar, kwa heshima na taadhima na kwa mujibu wa kanuni na ruhusa yenu Waheshimiwa, naomba sasa nimuombe Mhe. Hamza Hassan Juma yeye ndiye aliyeteuliwa kuwa wakala wa mgombea huyu, yeye itakuwa anajua yuko wapi.

Mhe. Hamza tuna jina la Spika amechaguliwa lakini hatunaye hapa, tunaomba utupatie huyo Spika sasa aje mbele ya hadhara hii ale kiapo na kuchukua nafasi yake. (*Makofi*)

(Hapa Mhe. Hamza alikwenda kumtafuta Mhe. Spika kwa ajili ya kula kiapo)

KIAPO CHA MHE. SPIKA

Katibu: Waheshimiwa Wajumbe, Mhe. Spika, anaingia naomba msimame.

Mhe. Zubeir Ali Maulid ninayo heshima kubwa kukuarifu kwamba Wajumbe wa Baraza hili Tukufu katika kutekeleza maamrisho ya Katiba na Kanuni za Baraza, na katika kutumikia haki na fursa waliyopewa, wajibu wa sheria wamekuchagua wewe uwe Spika wa Baraza hili. Kutokana na kuchaguliwa kwako huko, sasa nakuita wewe Mhe. Zubeir Ali Maulid uape kiapo cha uaminifu ikisha ukalie kiti cha Baraza hili ukiwa ni Spika. Mhe. Zubeir Ali Maulid karibu sana.

(Hapa Mhe. Spika aliapishwa na kukalia kiti)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kwanza kabisa naomba nisimame mbele yenu nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na afya na kutujumuisha pamoja katika ukumbi huu wa Baraza la Wawakilishi. Vile vile nimuombe Mwenyezi Mungu na kumshukuru kwa kujaalia uchaguzi kuwa wa salama salmini, uchaguzi uliofanyika tarehe 20 Machi, 2016.

Vile vile napenda kutoa shukurani kwenu Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kunipa imani na ridhaa yenu kuwa Spika wa nne wa Baraza la Wawakilishi, kiti ambacho nakirithi kutoka kwa Mhe. Pandu Ameir Kificho.

Vile vile nichukue nafasi hii kuishukuru sana familia yangu; mke wangu Fatma, watoto wangu Abdulkarim Zubeir, Hanifa Zubeir, Zahran Zubeir na Zahor Zubeir. Vile vile nichukue nafasi hii kumshukuru kaka yangu aliyenilea Kanal Mstaafu Hussein Hamza Nyange pamoja na familia yake. Nichukue nafasi hii pia kuwashukuru sana ndugu zangu wote wale tuliozaliwa tumbo moja na wale wa tumbo la Marehemu Sheikh Hamid Maulid Simai ambaye pia ndiye mwalimu wangu wa *qur-an* na madrasa. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wajumbe, lakini pia nisiwasahau rafiki zangu ambao walinishawishi kushiriki shughuli hizi za kisiasa na kunisifu kila nilipofanya vyema na kunipa moyo kila nilipoharibikiwa. Nichukue nafasi hii kuwashukuru walimu wangu walionisomesha tokea skuli ya msingi mpaka hapo nilipofikia. Bila ya kuwasahau walimu wangu wa madrasa Madrasatul-Khairiya ya Shauri Moyo na walimu wangu wa siasa ambao wengi wao ni katika jimbo ambalo sasa hivi linakuwa Jimbo la Shauri Moyo, lakini limekuwa na majina tofauti; Chumbuni, Kwamtipura hatimaye sasa hivi ni Shauri Moyo.

Waheshimiwa Wajumbe, nimalizie kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu lakini nikushukuruni sana kwa kazi nzuri muliyoifanya. Pia nichukue nafasi hii pamoja na kwamba Baraza hili ambalo nitakuwa ninaliongoza hivi sasa lina Wawakilishi ambao wengi wao mnatokea katika chama kimoja, basi huko nje tufanye kazi kwa uadilifu na kuwatumikia wananchi bila ya kujali itikadi zao za kisiasa. Kwani kufanya hivyo kutadumisha hii hali ya amani ambayo tunayo na hatimaye nchi tutaweza kuijenga kwa ushirikiano wa hali ya juu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wajumbe, baada ya shukurani hizo naomba sasa nichukue nafasi hii ili tuingie katika kazi inayofuata, kwa hiyo nimuombe Katibu aweze kunipa maelezo kuhusiana na shughuli inayoendelea.

KIAPO CHA UAMINIFU

Wajumbe wafuatao waliapishwa Kiapo cha Uaminifu na baada ya kumaliza walikaa katika nafasi zao.

1. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi
2. Mhe. Abdalla Ali Kombo
3. Mhe. Said Hassan Said
4. Mhe. Abdalla Maulid Diwani
5. Mhe. Ali Khamis Bakar
6. Mhe. Ali Salum Haji
7. Mhe. Ali Suleiman Ali
8. Mhe. Ame Haji Ali
9. Mhe. Amina Iddi Mabrouk
10. Mhe. Asha Abdalla Mussa
11. Mhe. Bahati Khamis Kombo
12. Mhe. Bihindi Hamad Khamis
13. Mhe. Chum Kombo Khamis
14. Mhe. Haji Omar Kheri

15. Mhe. Hamad Abdalla Rashid
16. Mhe. Hamida Abdalla Issa
17. Mhe. Hamza Hassan Juma
18. Mhe. Haroun Ali Suleiman
19. Mhe. Harusi Said Suleiman
20. Mhe. Hassan Khamis Hafidh
21. Mhe. Hidaya Ali Makame
22. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)
23. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)
24. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
25. Mhe. Juma Makungu Juma
26. Mhe. Khadija Omar Kibano
27. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed
28. Mhe. Khamis Juma Mwalim
29. Mhe. Lulu Msham Abdalla
30. Mhe. Machano Othman Said
31. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo
32. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti

Mhe: Spika: Waheshimiwa Wajumbe, Mjumbe anayefuata ni katika makundi maalum, kwa hiyo itabidi nimfate ili niweze kumuapisha. (*Makofi*)

(*Hapa Mhe. Spika alimfuata Mhe. Makame Said Juma kwa ajili ya kumuapisha)*

33. Mhe. Makame Said Juma
34. Mhe. Maryam Thani Juma
35. Mhe. Masoud Abrahman Masoud
36. Mhe. Mgeni Hassan Juma
37. Mhe. Mihayo Juma N'hunga
38. Mhe. Miraji Khamis Mussa
39. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri
40. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha
41. Mhe. Mohamed Ahmada Salum
42. Mhe. Mohammed Said Mohammed
43. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf
44. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame
45. Mhe. Mussa Ali Mussa
46. Mhe. Mussa Foum Mussa
47. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma
48. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa
49. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis
50. Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini
51. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf
52. Mhe. Nassor Salim Ali
53. Mhe. Omar Seif Abeid
54. Mhe. Panya Ali Abdalla
55. Mhe. Rashid Ali Juma
56. Mhe. Rashid Makame Shamsi
57. Mhe. Riziki Pembe Juma
58. Mhe. Saada Ramadhan Mwenda
59. Mhe. Said Omar Said
60. Mhe. Salama Aboud Talib
61. Mhe. Salha Mohammed Mwinyijuma
62. Mhe. Salma Mussa Bilal
63. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman
64. Mhe. Shaib Said Ali

65. Mhe. Shamata Shaame Khamis
66. Mhe. Shehe Hamad Mattar
67. Mhe. Simai Mohamed Said
68. Mhe. Suleiman Makame Ali
69. Mhe. Suleiman Sarahan Said
70. Mhe. Tatu Mohamed Ussi
71. Mhe. Ussi Yahya Haji
72. Mhe. Viwe Khamis Abdalla
73. Mhe. Wanu Hafidh Ameir
74. Mhe. Yussuf Hassan Iddi
75. Mhe. Zaina Abdalla Salum
76. Mhe. Zulfa Mmaka Omar
77. Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali

Katibu: Mhe. Spika, naomba kutoa taarifa kwamba kwa mujibu wa orodha ya shughuli za leo tumefikia mwisho wa shughuli zilizopangwa kwa kikao cha leo. Mhe. Spika, naomba kutoa taarifa.

Mhe. Spika: Ahsante sana Katibu. Waheshimiwa Wajumbe, kwanza nitoe shukrani zangu za dhati, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa mashirikiano na pia niwashukuru na niwapongeze kwa kuwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, baada ya kiapo ambacho mumekula hivi punde.

Waheshimiwa Wajumbe, kabla sijaahirisha nichukue nafasi hii kuwatambua baadhi ya wageni ambao wametufikia hapa leo. Waheshimiwa Wajumbe, naomba mtambue uwepo wa wageni wafuatao. Kwanza kabisa nitaanza na wageni wangu binafsi, ni wengi lakini nitawatambua wachache. *(Makofi)*

Naomba nimtambue mke wangu Fatma Abdalla Mzee. Pia, naomba nitambue uwepo wa wanangu Abdulkarim Zubeir, Hanifa Zubeir, Zahor na Zaharan wasimame kwa pamoja. *(Makofi)*

Vile vile, naomba nitambue uwepo wa mlezi wangu Kanal Mstaafu wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania Hussein Hamza Nyange, naomba asimame popote alipo. *(Makofi)*

Baada ya hao, naomba sasa nitambue uwepo wa wageni wa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais mteule. Naomba kumtambua mama Asha Balozi, naomba asimame popote alipo, simuoni. (*Makofi)*

Vile vile, naomba nimtambue ndugu Abdul Katabalo kama yupo hapa ukumbini asimame na yeye. Pia, naomba kutambua uwepo wa Mhe. Naibu Spika, mtaafu Mhe. Ali Abdalla Ali, naomba usimame popote ulipo *(Makofi)*

Pamoja na wageni wengine wote muliofika naomba kutoa shukrani zangu za dhati sana. Lakini kabla sijaahirisha naomba kumwita Mhe. Mwanasheria Mkuu ili atoe hoja. Mhe. Mwanasheria Mkuu, karibu.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja ya kutenga kando kanuni, kwa kuwa shughuli ambazo zilipangwa leo zimemaliza, hivyo, naomba kutoa hoja ya kuahirisha kikao hiki hadi siku ya Ijumaa saa 3:00 barabara za asubuhi. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsanteni sana Waheshimiwa Wajumbe, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Sasa naomba kuwahoji. Wale wote ambao wanaiunga mkono hoja iliyotolewa ili turudi tena siku ya Ijumaa saa 3:00 za asubuhi barabara wanyanyue mikono yao. Wanaokataa hiyo hoja. Waliokubali hiyo hoja wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Sasa naomba kuchukua nafasi hii kukiahirisha kikao hiki mpaka siku ya Ijumaa saa 3:00 za asubuhi barabara, ahsanteni sana.

(Saa 5:28 mchana kikao kiliahirishwa mpaka tarehe 01/04/2016 saa 3:00 za asubuhi)